DARASA LA SITA
MUHULA WA KWANZA 2018
KISWAHILI

Chagua jibu sahihi ili kujaza mapengo yaliyo katika kifungu hiki.

Mazingira ni uhai. Mazingira ni__1__ mazingira humpa mtu cheo kutokana na jinsi anapoishi__2__ Ni jambo __3__ kufurahisha sana kama kila mtu __4__ ya kuona mazingira yanawekwa__5__.

Hebu kwanza tuone nyumbani. Hapa__6__ mazingira yanapoanza. Kitanda kitandikwe vizuri, nyumba ifagiwe kwa usawa, madirisha__7__ili kuwe na hewa safi na jua__8__ hadi chumbani ili wadudu __9__ wahame.

Nyasi__10__karibu na nyumba ni lazima zikatwe ili kupunguza__11__. Takataka lazima__12__wakati zinapokusanywa ili wadudu kama__13__wasipate nafasi ya kutuletea uchafu na maradhi kama ya kuharisha. Mikebe iliyo wazi kandokando ya nyumba na__14__inaweza kujaa maji na kuwafanya wadudu hao wazaane lazima itupwe __15__.

1.	A. afia	B. avya	C. afya	D. afa
2.	A. kulivyo	B. palivyo	C. mlivyo	D. kuwavyo
3.	A. la	B. ya	C. cha	D. za
4.	A. angeona njaa	B. angechukua kamba	C. angechukua hatua	D. angelilila wembe
5.	A. masafi	B. safi	C. visafi	D. safisha
6.	A. ndimo	B. ndiko	C. ndipo	D. ndiposa
7.	A. zifunguliwe	B. wafunguliwe	C. ifunguliwe	D. yafunguliwe
8.	A. lipenye	B. ipenye	C. liingie	D. iingie
9.	A. mbaya	B. wabaya	C. baya	D. vibaya
10.	A. ndefu	B. ndevu	C. defu	D. refu
11.	A. umbu	B. ubu	C. mumbu	D. mbu
12.	A. izikwe	B. ipandwe	C. zizikwe	D. zipandwe
13.	A. konokono	B. insi	C. chawa	D. nzi
14.	A. ambayo	B. ambazo	C. ambao	D. ambawo
15.	A. bali	B. mbali	C. mbalimbali	D. mbari

Kutoka swali la 16 hadi la 30 chagua jibu lililo sahihi.

16. Jibu la "Ndoto njema" ni_____
A. majaliwa B. jaala
C. ya mafanikio D. wa salmini

17. "Rafiki yangu ni kunguru" maana yake ni_____
A. mwerevu B. mwoga
C. mkaidi D. mlafi

18. Barabara hii imenyoka_____
A. mwaa! B. pa!
C. twaa! D. chumbwi!

19. ***Tegua kitendawili hiki.***
Nameza lakini sishibi
A. maji B. mate
C. maziwa D. uji

Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.O. Box 8076 – 00200, Nairobi Tel: +254202319748 | +254 711 88 22 mail: infosnkenya@gmail.com Website: www.schoolsnetkenya.com

20. ***Chagua sentensi iliyo sahihi***
A. Mama ameenda kwa mkutano
B. Mtoto hakuji kukula chakula
C. Ana vitabu kumi na mbili
D. Jino jingine limeng'olewa

21. ***Kamilisha methali***
Kidole kimoja hakivunji_____
A. chawa
B. kuni
C. kalamu
D. nyumba

22. Neno lipi lililoendelezwa sahihi?
A. asubuhi B. chukuwa
C. wakisha D. ghorofa

23. ***Andika tarakimu hii kwa maneno:-***
199,717
A. laki moja tisaini na sita elfu mia saba kumi na saba
B. laki moja tisaini na tisa elfu, mia saba kumi na saba
C. laki kumi na tisa elfu tisa sabini na saba
D. elfu kumi na tisa mia tisa na kumi na saba

24. Ni kiungo kipi kinachowekwa katika chai?
A. karafuu
B. dania
C. tangawizi
D. kitunguu maji

25. Ala hii ya muziki inaitwa

A. gitaa
B. ngoma
C. tari
D. parapanda

26. Ni sentensi ipi iliyotumia 'amba kwa usahihi?
A. mtoto ambaye aliyeshinda ni huyu
B. ulimi ambayo unauma ni huu
C. maga ambazo ni mbaya zishikwe
D. wanafunzi ambao hijitahidi hufaulu

27. Aina ya meli inayotumika katika shughuli za kivita ni__
A. bomu B. manowari
C. kifaru D. singe

28. ***Tumia kiulizi -pi kujaza pengo.***
Ni mazingira_____yaliyo mema
A. yapi B. yupi
C. ipi D. wapi

29. Kifaranga huyu_____aliyeibwa
A. ndicho B. ndiyo
C. ndio D. ndiye

30. ***Tumia -ngine kujaza nafasi.***
Tunda_____limeoza
A. lingine B. jingine
C. ingine D. nyingine

Soma kifungu kifuatacho kisha uyajibu maswali 31-40.

Maina alisoma kwa shida. Wakati mwingine alienda shule bila ya kula chochote, hata wakati wa jioni alikosa chajio. Kila siku yeye alikuwa tayari kuishi maisha magumu pamoja na ninaye na yote aliyokuwa akiambiwa na mama yake aliyazingatia.

Mtoto huyu alisoma kwa bidii. Kuwe kuna mvua au jua, baridi au joto. Maina alikuwa tayari kwa lolote lile. Shuleni alifanya bidii sana ingawa alikuwa na shida. Mwalimu wa nasari alimpenda sana kwa bidii na heshima aliyokuwa nayo.

Alipojiunga na shule ya msingi hakuna mtoto aliyemshinda katika darasa la kwanza. Alikuwa wa kwanza katika kila somo. Mvulana huyu alipendwa na walimu wote. Kamati ya shule iliamua kumsaidia kwa nguo na karo.

Alipofika darasa la nane ndiye aliyekuwa nyota wilayani kote. Alikuwa wa kwanza kijijini mwao katika shule ya upili ya kitaifa.

Maina alipata msaada wa masomo kutoka kwa serikali na huko pia alifaulu na kuingia chuo kikuu ambako alihitimu shahada ya digrii.

Leo hii Maina ni meneja kazini. Amemnunulia mama yake shamba na akamjengea nyumba kubwa. Amenunua gari la starehe. Kweli, mvumilivu hula mbivu

31. Maina aliishi maisha gani?
A. ya raha B. ya kucheza
C. ya shida D. ya ukorofi

32. Neno **ninaye** limepigwa mstari lina maana_____
A. shangazi yake
B. mama yake
C. baba yake
D. nyanya yake

33. "Chajio" ni chakula cha_____
A. asubuhi B. mchana
C. jioni D. kila siku

34. Maina alikuwa _____shuleni
A. mvivu B. mtukutu
C. mwenye tamaa D. mwenye bidii

35. Shule ya nasari pia yaweza kuitwa_____
A. chekechea B. chuo
C. msingi D. sekondari

36. Maina alikuwa na haya yote isipokuwa_____
A. bidii B. heshima
C. uzembe D. uvumilivu

37. Kwa nini mwalimu wa nasari alimpenda Maina?
A. alikuwa na bidii na uzembe
B. alikuwa na heshima na bidii
C. alikuwa mvivu na mwenye heshima
D. alikuwa mtiifu na mwenye kiburi

38. Karo ni malipo shuleni. Malipo ya usafiri ni____
A. kiingilio B. riba
C. nauli D. kiongozi

39. Maneno "ndiye aliyekuwa nyota wilayani kote" yana maana kuwa
A. alimetameta kama nyota
B. alimulika wilaya ikapata mwangaza
C. aliwashinda watoto wa darasa lake
D. alikuwa wa kwanza katika wilaya nzima

40. "Mvumilivu hula mbivu" ni_____
A. methali B. tashbihi
C. istiara D. tanakali za sauti

Soma kifungu kifuatacho kisha uyajibu maswali 41-50.

Ni jambo la kusikitisha mno tunapoona vijana wanavyojitumbukiza katika janga la kutumia au kuuza dawa za kulevya kwani vijana ndio nguzo za matarajio ya taifa lolote. Wimbi hili la kutumia mihadarati limeingia kwa kasi kubwa na yote ni kwa sababu ya ukosefu wa kazi na ukosefu wa mwelekeo na maongozi kwa vijana hawa. Zaidi ya haya, wale matajiri walafi ndio wanaopotosha vijana kwa kuwaingiza katika janga la kuuza mihadarati kama vile bangi. Hii ni kwa vile vijana wanavutiwa na malipo ya juu wanayolipwa na wepesi wa kazi hiyo.

Bila shaka muuza mafuta mazuri lazima ajipake ili kuwavutia wanunuzi. Vivyo hivyo, muuza mihadarati ni lazima atumie angalau kwa kiasi kidogo mwanzoni kabla ya kitendo hicho kuwa ni uraibu asiyoweza kuepuka kwa hali yoyote.

Visa vya vijana waliojiangamiza wenyewe ni vingi na vya kuhusunisha. Wanamalizika wakiwa hohehahe na mwishowe tutakuwa na taifa la wapumbavu lisilokuwa na mawazo wala msimamo.

41. Mwandishi anasikitika kwa sababu:-
A. ya janga la njaa
B. ugonjwa umeenea
C. vijana wanapotea
D. dawa za kulevya ni ghali

42. Ni ipi si sababu za vijana kutumia dawa za kulevya?
A. ukosefu wa elimu
B. ukosefu wa kazi
C. ukosefu wa maongozi
D. marafiki wabaya

43. Vijana wanaingizwa katika shughuli za kuuza dawa za kulevya na_____
A. wazazi B. matajiri
C. viongozi D. polisi

44. Vijana wanakubali kuuza dawa za kulevya kwa sababu ya_____
A. kuipenda kazi hiyo
B. kutotaka kazi
C. malipo mazuri
D. kulazimishwa

45. Dawa za kulevya pia zajulikana kama_____
A. mihadarati
B. mkwasi
C. maradhi
D. zahanati

46. Matarajio ya nchi yoyote kwa vijana ni_____
A. kujenga nchi
B. kutumia dawa za kulevya
C. kuharibu nchi
D. kusambaza dawa za kulevya

47. Twasema, mlafi kama_____
A. simba B. ndovu
C. kuku D. fisi

48. Vijana hupewa mwelekeo na watu hawa isipokuwa__
A. wazazi
B. makasisi
C. walevi
D. walimu

49. Kinyume cha vijana ni_____
A. wasichana
B. wazee
C. wavulana
D. wanawake

50. Kichwa kinachofaa taarifa hii ni_____
A. Vijana wapumbavu
B. Vijana na dawa za kulevya
C. Matajiri
D. Kuwa masikini